



CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA WAHITIMU WA VYUO VYA ELIMU YA JUU “Badili Changamoto kuwa Fursa”

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anawatangazia wahitimu wote wa elimu ya juu kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeandaa mafunzo ya ujasiriamali yatakayotolewa katika mikoa kumi na moja ya Tanzania (Tanzania Bara na Zanzibar) mwezi Oktoba na Novemba mwaka 2021. Mafunzo haya yanatolewa kama sehemu ya huduma kwa jamii inayofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

LENGO KUU LA MAFUNZO

Kuwapatia vijana uelewa, taarifa, maarifa, ujuzi na uwezo wa kuainisha fursa zinazowazunguka na kuweza kuzitumia fursa hizo kwa kuanzisha biashara na kutoa ajira kwa ajili yao na wenzao na hivyo kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla.

MALENGO MAHUSUSI

- Kujenga uwezo na tabia ya kutumia taaluma zao kutambua matatizo na changamoto kama fursa za kibiashara.
- Kukutana na kujifunza kutoka kwa wajasiriamali wazoeifu kutoka kwenye sekta mbalimbali.
- Kutengeneza mipango ya biashara ambayo itawasaidia kutafuta mitaji.
- Kuwaunganisha vijana wenye mawazo mazuri ya ujasiriamali na watoa huduma za kifedha, teknolojia na uatamizi.

WALENGWA

Mafunzo haya yanawalenga vijana wahitimu wa Vyuo vya Elimu ya Juu kuanzia Diploma wenye nia ya kujiajiri.

MUDA WA MAFUNZO

Mafunzo haya yatatolewa katika makundi ya watu wasiozidi 50 kwa darasa kwa muda wa siku nne mfululizo kwa kila mkoa uliotajwa.

RATIBA YA MAFUNZO

Mahali	Tarehe za Mafunzo	Mwisho wa Kujisajili
Dar es Salaam	04/10/2021 - 14/10/2021	29/09/2021
Morogoro	06/10/2021 - 14/10/2021	29/09/2021
Mtwara	06/10/2021 - 14/10/2021	29/09/2021
Tanga	06/10/2021 - 14/10/2021	29/09/2021
Dodoma	18/10/2021 - 21/10/2021	13/10/2021
Kigoma	18/10/2021 - 21/10/2021	13/10/2021
Mjini Magharibi	18/10/2021 - 21/10/2021	13/10/2021
Geita	20/10/2021 - 28/10/2021	15/10/2021
Kilimanjaro	25/10/2021 - 28/10/2021	20/10/2021
Njombe	25/10/2021 - 28/10/2021	20/10/2021
Kusini Pemba	01/11/2021 - 04/11/2021	28/10/2021

GHARAMA ZA MAFUNZO

Washiriki hawatalipa ada. Wanaotoka mbali watajigharamia usafiri wa kwenda na kurudi na malazi.

JINSI YA KUSHIRIKI

Kujisajili, tembelea tovuti ya Chuo Kikuu cha DSM na kujaza maombi kwa kupitia fomu iliyo katika tovuti ya <http://udsm-mafunzo.ac.tz>

Kwa changamoto yoyote wasiliana nasi kwa kutuma barua pepe kwenye anuani udiec@udsm.ac.tz na/au WhatsApp no. +255-734-669-818.

Kwa Mawasiliano zaidi:

Mkurugenzi, Kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali (UDIEC)
S.L.P 110099 Dar es Salaam
Tel: +255-734-669-818 +255-758-461-028.
Email: udiec@udsm.ac.tz.

“WAHI KUJIANDIKISHA NAFASI NI CHACHE”

Hekima ni Uhuru

www.udsm.ac.tz